THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

MUDA: Saa 2 2006/10/13 Mchana

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Bismillahir -- Rahmanir – Rahiim

## SEHEMU A: SUNNA NA HADITH (alama 10)

1. Chagua jibu lililo sahihi kwa kila swali (i) – (x) kisha andika herufi ya jibu hilo kando ya namba ya swali husika katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Katika wakati wa Mtume (S.A.W.) Hadith hazikuandikwa kwa sababu

A Mtume aliwakataza Maswahaba kuandika Hadith
B Maswahaba walijishughulisha sana na kusoma na kuihifadhi Qur-an
C Waliweza tu kufuata matendo ya Mtume (S.A.W.)
D Hapakuwa na swahaba aliyejua kusoma na kuandika
E Wafuasi hawakujua kusoma wala kuandika.

(ii) Uandishi wa Hadith ulipewa uzito mdogo wakati wa Mtume (S.A.W.) kwa sababu ipi?

A Maswahaba walikuwa karibu na Mtume wakati wote
B Maswahaba walihifadhi Hadith nyingi zaidi kuliko waumini wengine
C Hadith nyingi zilibakia katika matendo na vifua vya maswahaba
D Maswahaba waliokuwa karibu na Mtume walikuwa wachache mno
E Hadith hazikuonekana kama sehemu muhimu ya mafundisho ya Uislamu.

(iii) Katika mwaka wa 11 AH hadi 101 AH matatizo mengi ya kipindi hicho yalitatuliwa kwa hukumu za misingi ipi?

A Sheria za Qur-an
B Maamuzi ya Shura
C Hukumu za watawala wa Banu Umayah
D Sheria za Mahakama zilizotungwa na maswahaba
E Hukumu za Hadith zilizohifadhiwa na Maswahaba.

(iv) Kiongozi aliyechukua dhima ya kuchuja na kuziandika Hadith zilizo sahihi alikuwa nani?

A Seyyidna Ali ibn Abu Talib aliyefariki 40 AH
B Tufayli Aamir bin Wathilah aliyefariki 110 AH
C Ibn Abass aliyefariki 681 AH
D Ummar bin Abdul – Aziz (99 – 101 AH)
E Kila kiongozi aliyeongoza Dola ya Kiislamu.

(v) Kitabu cha mwanzo cha Hadith kilichoandikwa na kuwekwa kwa utaratibu mzuri ni cha mwandishi yupi?

A Abuu Hanifa an Numan bin Thabit
B Maamar bin Rashid
C Saad bin Abu Ubaidah
D Iman Malik bin Anas
E Ibn Majah.

(vi) Hadith maudhui ni zile zenye sifa zifuatazo:

A Kukosekana kwa taadil kukiri msimulizi mwenyewe
B Kukamilika kwa Isnad, rawy na matin
C Kukamilika kwa rawy na matin
D Tamko la matin ya Hadith kuwa jepesi
E Kukamilika kwa matin na taadil.


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

(vii) Ipi ni maana ya Isnad katika elimu ya Hadith?

A Kutegemeza kitu juu ya kitu kingine
B Maneno yaliyomo ndani ya Hadith pamoja na wapokezi wake
C Hadith ambayo imekamilika kwa sharti zake zote
D Hadith iliyoshikamana kuanzia mwanzo hadi mwisho wake kumfikia Mtume (S.A.W.)
E Kitu au suala linalozungumzwa katika Hadith.

(viii) Hadith sahihi inatambulika kwa sifa ipi?

A Imeandikwa na wana-Hadith wengi
B Sanadi yake imeshikamana kwa kunukuliwa na mnukuaji muadilifu na muhifadhi mzuri.
C Iliyohifadhiwa na watu katika wakati wa Maswahaba
D Hadith ambayo haipingani na Qur-an tukufu.
E Imesheheni aya na sura za Qur-an tukufu.

(ix) Hadith dhaifu hudhihirika kwa sifa ipi?

A Haina nguvu mbele ya wanazuoni
B Matin yake haina mlolongo wa mwaat
C Imetokana na wahifadhi dhaifu walioisimulia
D Kutofahamika Rawi mmoja katika sanadi
E Haikuenezwa kwa wanazuoni mashuhuri.

(x) Kitabu cha pili kwa usahihi wa Hadith ni kipi?

A Hadith Qudus
B Jamuiatu Tirmidh
C Sunan Ibn Majah
D Sahihi Bukhar wa Muslim
E Sunan Abun Daudi

## SEHEMU B: QUR-AN (alama 15)

2. Chagua kutoka Orodha B kifungu kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka Orodha A.

**Orodha A**

(i) Amri ya kuitangaza dini ya Allah inatokana.

(ii) Na lau Muhammad angeongeza baadhi ya maneno (69:43-49) basi tungemchukua kwa mkono wa kuume.

(iii) Hakika sisi tumeiteremsha Qur-an hii katika usiku wenye baraka. Hakika sisi ni wenye kuiteremsha.

(iv) Na hakuwa jamaa yenu kuwa ni mwendawazimu.

(v) Elimu ni jambo la msingi katika Uislamu na katika uongozi wowote pia katika kutafuta elimu lazima kupata mashaka (19:122).

(vi) Wakasema makafiri haikuwa (hii Qur-an) ila uongo aliouzua na wakamsaidia watu wengine, hakika amekuja na dhuluma na uongo (25:5).


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

(vii) Ameiteremsha Jibril mwenye uaminifu juu ya moyo wako ili uwe muonyaji (26:193-194).

(viii) Sisi ndio tulioiteremsha Qur-an na sisi ndiyo tutakaoilinda (15:9).

(ix) Nawakumbusha pale Mtume alipomwambia mmoja wa wake zake neno la siri basi alipomueleza sehemu na kuacha sehemu alimuuliza nani aliyekueleza jambo hili? (66:3).

(x) Na lau wangekusanyika majini na watu kuleta mfano wa hii Qur-an wasingeweza na hata kama wengine wangewasaidia wengine (17:88).

(xi) Hawazingatii hii Qur-an au ndani ya mioyo yao mna vifuniko.

(xii) Wakasema ngano za watu waliotangulia ameziandika basi anasomewa asubuhi na jioni (25:5).

(xiii) Au angeteremshiwa hazina au angekuwa na shamba ambalo anakula ndani yake wakasema madhalimu hamumfuati ila mtu aliyerogwa (25:8).

(xiv) Sisi tu ndio tulioiteremsha hii Qur-an katika usiku wenye baraka na hakika sisi ni waonyaji (44:3).

(xv) Haikuwa kwa kiumbe kumsemesha Mwenyezi Mungu ila kwa wahay au nyuma ya pazia au humpelekea mjumbe basi humfikishia wahay kwa idhini yake kwa yale ayatakayo - hakika yeye ni Mtukufu mwenye hekima (45:51).

(xvi) Na hivyo hivyo tulikupelekea Jibril kwa amri yetu, ulikuwa hujui nini kitabu.

**Orodha B**

A Madai ya makafiri dhidi ya Qur-an.

B Mtume ameipokea Qur-an kwa njia ya wahay.

C Qur-an itabaki katika asili yake.

D Qur-an ni neno la Allah "SW".

E Qur-an (26:215–216).

## SEHEMU C: TAWHIID (alama 15)

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba zinazohusika tu katika kijitabu chako cha kujibia.
**Mfano:** Tafsiri ya Surat Masad ni:

(i) Ndani ya shingo yake mna kamba madhubuti.

(ii) Atauingia moto wenye muwako mkali.

(iii) Imeangamia mikono ya Abii Lahabi na yeye mwenyewe.

(iv) Na mkewe ambaye amebeba kuni (za fitina).

(v) Haitamfalia kitu mali yake aliyoichuma.
**Jawabu:** (iii) (v) (ii) (iv) (i)

(a) (i) Yeye ndiye wa mwanzo na wa mwisho na kwa dhahiri na kwa siri na yeye kwa kila kitu ni mjuzi.


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) Anaingiza usiku katika mchana na huingiza mchana katika usiku na yeye ni mjuzi wa yaliyo katika nyoyo.

(iii) Yeye ndiye aliyeumba mbingu na ardhi katika siku sita.

(iv) Yeye ndiye mwenye ufalme wa mbinguni na ardhini, ndiye mwenye kuhuisha na kufisha na yeye ni mweza wa kila kitu.

(v) Kwake yeye ufalme wa mbinguni na ardhini na kwa Mwenyezi Mungu tu yanakorejea mambo.

(b) (i) Wala kwa wale wanaokufa hali ya kuwa makafiri.

(ii) Hao tumewaandikia adhabu yenye kuumiza.

(iii) Toba ya kweli ni kwa wale wanaofanya uovu kwa ujinga kisha wakatubu baada ya muda mfupi.

(iv) Wala hapana toba kwa wale wanaofanya maovu mpaka yakamfika mauti mmoja wao akasema sasa nimetubu.

(v) Basi hao ndio atakaowasamehe Mwenyezi Mungu na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi mwenye hekima.

(c) (i) Ishara zilizo wazi kabisa zinaonekana kwa kila mtu mwenye akili.

(ii) Maumbile ya mbingu na ardhi na maumbile yote.

(iii) Kwa kutafakari ishara mbali mbali zilizomzunguka.

(iv) Kuyakinisha pasi na shaka yoyote juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.

(v) Jambo la kwanza kwa mwanadamu mwenye akili.

## SEHEMU D: FIQH (alama 30)

4. Jibu kwa ufupi kwa kujaza nafasi zilizo wazi katika maswali (i) – (xv). Andika neno au maneno yanayokosekana tu katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Miongoni mwa nguzo za funga ni (a) .......... na (b) ............

(ii) Najisi nzito inaweza kuondoshwa kwa (a) .......... na najisi nyepesi kwa (b) ...........

(iii) Sharti ya sala ya kuomba mvua ni (a) ................ na (b) .................

(iv) Miongoni mwa sharti za funga ni (a) ............., (b) ............ na (c) .................

(v) Katika mirathi mtoto wa kike hupata (a) ............ akiwa peke yake au (b) .............. wakiwa (c) ................ au (d) ....................

(vi) Kuoa ni wajibu ikiwa (a) ............ na ni haramu ikiwa (b) ......................

(vii) Eda ya mwanamke aliyeachwa ni (a) .............. aliyefiwa na mumewe ni (b) ............ na wale waliokuwa hawana hedhi (c) .................. na mwenye mimba ni (d) ................

(viii) Wanaosifiwa kwa sifa ya Mutakiina huwa na sifa zifuatazo (a) ........... (b) ................ (c) .................. na (d) ......................

(ix) Matendo yanayokamilisha amali ya Hija ni (a) .............., (b) ............... (c) ...............

(x) Taqwa inayopatikana katika amali ya funga ni (a) ........... (b) .............. (c) ...............



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(xi) Tofauti ya zakat na sadakat ni (a) ................, (b) ...................... na (c) ....................

(xii) Maiti wa kike wa Kiislamu atafukuliwa pindi (a)................... na (b) .........................

(xiii) Mazao ya kumwagilia maji shambani hutolewa zakat kwa kiwango (a) ............... na yale yaliyonyeshewa mvua hutolewa zakat (b) ...................

(xiv) Adhabu ya mtu mlevi ni (a) ......... na ya mtu mzinifu ghaira muhswan na ya yule muhswan ni (b) ......................

(xv) Zakat ya ngamia kumi (a) ................. na zakat ya ng'ombe thelathini ni (b) ................

## SEHEMU E: TAREKH (alama 30)

5. Chagua neno au kifungu cha maneno (1) – (32 ili ukamilishe kauli (a – o) kwa usahihi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Uhud | 17. | Mkataba wa Hudaibiya |
| 2. | Hamza | 18. | Abdullah bin Zubeir |
| 3. | Nuh | 19. | Alitoa rai ya kuchimbwa handaki |
| 4. | Adam | 20. | Ahzab |
| 5. | Saqifa bani Saida | 21. | Jaffar bin Abu Talib |
| 6. | Waraqah bin Naufal | 22. | Torati |
| 7. | Kabila mbili | 23. | Bibi Khadija |
| 8. | Jabal Safa | 24. | Suleiman Alfarisy |
| 9. | Asmaa | 25. | Watupa Mishale |
| 10. | Daru Nadwa | 26. | Kumuunga mkono |
| 11. | Abubakar | 27. | Vipengele vya suluhu ya Hudaibiya |
| 12. | Ghar thaur | 28. | Answar |
| 13. | Muhammad | 29. | Abuu Lahab |
| 14. | Abuu Jandal | 30. | Habasha |
| 15. | Abuu Ayub | 31. | Mtume |
| 16. | Madina | 32. | Seydina Omar |

**MASWALI**

(a) Mtume alipopewa amri ya kulingania Jahara alipanda .................... katika mkusanyiko huo alikuwepo ami yake ........................

(b) Katika vita vya ................ aliuawa ................. kwa kukatwa katwa kikatili.

(c) Mtume wa pili baada ................ ni .....................

(d) .................. yalikutana katika ... ......... kwa ajili ya kupanga njama ya kumuua Mtume.

(e) .................... ndiye aliyewahudumia katika ................ mara tu baada ya kutoka nyumbani kwake.

(f) Baada ya kumsimulia mkewe .................. alimpeleka kwa .......... ambaye alikuwa ni ...............



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(g) .................. hakukubaliana na ..................... ambavyo vilikuwa vinawadhalilisha Waislamu.

(h) Mtume alipofika ................ alifikia kwenye nyumba ya .........................

(i) .................. alisilimu baada ya kutiwa saini ...............................

(j) Baada ya kutawafu Mtume ................... walikutana katika .........................

(k) Kabla ya vita vya ..................... swahaba mmoja alitoa rai ya .........................

(l) Kiongozi wa Hijra ya mwanzo kuelekea ..................... ni .............................

(m) Katika kitabu cha ..................... ametajwa ..........................

(n) .............................. ndiye aliyekuwa ........................... kwa kila alichosema.

(o) Katika vita vya Uhudi kiongozi wa ....................... ni ........................



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org